UHIFADHI // UTALII // MAENDELEO YA JAMII

# FARU

*Linatolewa na **Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro***

Toleo la Juni, 2025



## NCAA Yang'ara Tuzo za WTA 2025

### Kivutio bora cha Utalii Afrika 2025

www.ncaa.go.tz
@visitngorongoro

# ASANTE KWAKO,

## TUMESHINDA!


KIVUTIO BORA CHA UTALII AFRIKA
TUZO ZA WORLD TRAVEL AWARDS 2025




Visit NGORONGORO
for Unforgettable Experiences!

www.ncaa.go.tz
@visitngorongoro

TANZANIA
Unforgettable!




# YALIYOMO


01 ENEO LA HIFADHI YA NGORONGORO; KIVUTIO NAMBA MOJA CHA UTALII BARANI AFRIKA 2025

03 CHEO NI DHAMANA NA KINAKUJA NA MAJUKUMU; BALOZI DKT. PINDI CHANA

05 KAMISHNA BADRU ALA KIAPO CHA MAADILI

06 MAONESHO YA UTALII NA UWEKEZAJI ZANZIBAR YAWA FURSA KWA WANANCHI KUJUA VIVUTIO VYA UTALII NGORONGORO

08 NCAA ILIVYONOGESHA HAMASA YA UTALII WIKI YA UTUMISHI WA UMMA, DODOMA

10 MAPADRI KANISA KATOLIKI SINGIDA WAIASA JAMII KUTUNZA MAZINGIRA NA KUHAMASISHA UTALII WA NDANI

11 WAONGOZA UTALII WATOA KONGOLE KWA NCAA MABORESHO YA BARABARA KUELEKEA MSIMU WA UTALII

12 NIDHAMU NA UADILIFU NI NYENZO MUHIMU KATIKA UTENDAJI KAZI KIJESHI; CP WAKULYAMBA

14 DKT. KIJAJI AZINDUA CHANJO YA MIFUGO NGORONGORO











KARIBU
NGORONGORO


**MAMLAKA YA HIFADHI YA ENEO LA NGORONGORO (NCAA)**
S.L.P 1 Ngorongoro Kreta,
Arusha - Tanzania
Simu: +255 734 160 014/15
Barua pepe: cc@ncaa.go.tz
Tovuti: www.ncaa.go.tz




# ENEO LA HIFADHI YA NGORONGORO; KIVUTIO NAMBA MOJA CHA UTALII BARANI AFRIKA 2025.

Na **Hamis Dambaya, NCAA.**



“

Tumepokea kwa furaha na hamasa kubwa tuzo hii, kwetu Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro imetuongezea ari ya kufanya kazi kwa juhudi na maarifa ili kulinda hadhi tuliyoipata na tunawashukuru watu wote waliotupigia kura kote ulimwenguni kwa kuwa bila kura zao tusingeweza kushinda.

**Abdul-Razak Badru**
Kamishna wa Uhifadhi, NCAA

Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro limeibuka kinara katika kinyang’anyiro cha kuwania tuzo ya kuwa Kivutio bora cha utalii Barani Afrika kwa mwaka 2025 (Africa’s Leading Tourist Attractions) inayotolewa na mtandao wa World Travel awards (WTA).

Tukio la kukabidhiwa tuzo hiyo ilifanyika tarehe 28 Juni, 2025 katika hoteli ya Johari Rotana jijini Dar es Salaam baada ya kushindanishwa na vivutio vya nchi mbalimbali Afrika.

Akielezea ushindi huo, Kamishna wa Uhifadhi wa Mamlaka ya Hifadhi ya eneo la Ngorongoro Abdul-Razak Badru amesema kuwa tuzo hiyo ni heshima kwa Mamlaka na nchi kwa ujumla.

“Tumepokea kwa furaha na hamasa kubwa tuzo hii, kwetu Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro imetuongezea ari ya kufanya kazi kwa juhudi na maarifa ili kulinda hadhi tuliyoipata na tunawashukuru watu wote waliotupigia kura kote ulimwenguni kwa kuwa bila kura zao tusingeweza kushinda”. alisema Kamishna Badru

Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro imeshinda tuzo hiyo baada ya kushindanishwa na vivutio vingine vya utalii Afrika vikiwemo Harberespoort Aerial Cable way, V&A Water front, Table Mountain na Kisiwa cha Robens kutoka Afrika Kusini, Pyramids of Giza cha Misri na Ziwa Malawi na vingine.



“Ngorongoro ni kivutio pekee duniani ambacho kina hadhi tatu za Kimataifa zinazotambuliwa na UNESCO, tuna Wanyama wakubwa maarufu watano “The Big Five’ ambao ni Faru, simba, tembo, nyati na chui sambamba na Wanyama wengine wengi ambao unaweza kuwaona kwa pamoja ndani ya muda mfupi”, alisema Kamishna Mwandamizi Msaidizi anayeshughulikia huduma za utalii Mariam Kobelo.

“Tuna makumbusho ya kihistoria katika Bonde la Olduvai lilipogunduliwa Fuvu la Binadamu wa kwanza ‘Zinjanthropus’. Vivutio vingine ni pamoja na kuna Nyayo a Binadamu wa kale aliyeishi zaidi ya miaka milioni 3.7 iliyopita, mlima Lolmalasin ambao ni wa tatu kwa urefu Tanzania, mchanga unaohama, tambarare za Ndutu ambazo ni mazalia ya Nyumbu wanaohama, maporomoko ya maji ya endoro, mapango ya tembo na vivutio vingine vingi” ”Mariam Kobelo, Kamishna Mwandamizi Msaidizi anayeshughulikia Huduma za Utalii na Masoko alisisitiza.

Mafanikio ya kupata hadhi mbalimbali za kimataifa pamoja na tuzo ya kivutio bora cha utalii Afrika mwaka 2025 yametokana na juhudi kubwa zinazofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kutokana na hamasa kubwa aliyonayo katika sekta ya uhifadhi na utalii hasa kupitia filamu ya Tanzania, The Royal Tour na Amazing Tanzania.

Akizungumza wakati wa utoaji wa tuzo hizo Waziri wa Maliasili na Utalii Balozi Dkt. Pindi Chana ameeleza kuwa tuzo ambazo Tanzania imezipata ni heshima kwa taifa. “Tuzo hii na nyingine tulizozipata kama nchi ni mahsusi kwa Rais wetu mpendwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye yeye ndiye kinara namba moja katika kusimamia uhifadhi, utalii na maendeleo ya watanzania, tuhakikishe tunalinda mafanikio haya kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho”. alisema Mhe. Balozi Dkt. Chana.

Hii ni mara ya pili kwa eneo la Hifadhi ya Ngorongoro kushinda tuzo ya kuwa kivutio bora cha utalii barani Afrika ambapo mara ya kwanza ilishinda tuzo hiyo mwaka 2023.



**Kamishna wa Uhifadhi NCAA, Bw. Abdul-Razaq Badru (kushoto) akiwa katika mkutano na waandishi wa habari jijini Arusha.**



**Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi NCAA Jenerali Venance Mabeyo (Mstaafu) (kulia) akimkabidhi Kamishna wa Uhifadhi NCAA, Bw. Abdul-Razaq Badru tuzo ya kivutio bora cha utalii Afrika 2025.**




# CHEO NI DHAMANA NA KINAKUJA NA MAJUKUMU; BALOZI DKT. PINDI CHANA.

Na **Kassim Nyaki, Arusha.**

> “
>
> Ni matumaini yangu kuwa viongozi wote mliovaa vyeo leo mtakuwa chachu ya kufanya kazi kwa kujituma na kuonesha mfano wa kuigwa kwa Maafisa na Askari mnaowaongoza, juhudi zenu ndiyo zitakazochangia kulinda na kuhifadhi eneo la Ngorongoro na kuendelea kuwa kivutio kwa wageni wanaotembelea.
>
> **Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb)**
> Waziri wa Maliasili na Utalii

Waziri wa Maliasili na Utalii Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb) amewavisha cheo manaibu kamishna wawili na kushuhudia uvishwaji vyeo kwa makamishna wasaidizi waandamizi watano waliovishwa vyeo na mwenyekiti wa bodi ya Wakurugenzi NCAA Jenerali Venance Mabeyo (Mstaafu) na kuwasisitiza kuwa vyeo hivyo ni dhamana na vinakuja na majukumu.

Waliovishwa Cheo na Mhe. Waziri ni Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi Joas John Makwati aliyepandishwa cheo kuwa Naibu Kamishna wa Uhifadhi anayesimamia Uhifadhi, utalii na Maendeleo ya Jamii na Naibu Kamishna wa Uhifadhi Aidan Paul Makalla anayesimamia Huduma za Shirika NCAA.

Kwa upande wa makamishna waliovishwa vyeo na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi NCAA Jenerali Venance Mabeyo (mstaafu) ni Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi anayesimamia idara ya Mipango na uwekezaji, Gasper Stanley Lyimo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi Paul Geofrey Shaidi anayesimamia Kitengo cha huduma za Sheria, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi Charles Marwa Wangwe anayesimamia Idara ya Uhasibu na fedha.

Wengine ni Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi Godwin Felician Kashaga anayesimamia Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, na Afisa Uhifadhi Mkuu Daraja




la kwanza Mariam Kobelo anayesimamia idara ya Huduma za Utalii na masoko ambaye amepandishwa kuwa Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi.

Baada ya kuwavisha vyeo hivyo waziri wa Maliasili na Utalii Mh. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb) amewaelekeza maafisa hao kufanya kazi kwa bidiii na weledi mkubwa katika kutekeleza majukumu yao kwa kuwa cheo ni dhamana na kinakuja na majukumu.

“Ni matumaini yangu kuwa viongozi wote mliovaa vyeo leo mtakuwa chachu ya kufanya kazi kwa kujituma na kuonesha mfano wa kuigwa kwa Maafisa na Askari mnaowaongoza, juhudi zenu ndiyo zitakazochangia kulinda na kuhifadhi eneo la Ngorongoro na kuendelea kuwa kivutio kwa wageni wanaotembelea” ameongeza Balozi Chana.

Kamishna wa Uhifadhi NCAA Abdul-Razak Badru ameeleza kuwa kwa sasa watumishi wote wa NCAA wameshapatiwa mafunzo ya kijeshi kutoka mfumo wa awali wa kiraia na kuwa mamlaka hiyo itahakikisha inatumia rasilimali ya watumishi waliopo kuongeza nguvu ya kuhifadhi, kulinda, kuendeleza jamii na kuboresha miundombinu ya utalii.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Bodi ya NCAA Jenerali, Venance Mabeyo (mstaafu) ameeleza kuwa mafanikio ya Ngorongoro yanategemea uadilifu na uwezo wa viongozi wake na kuwaasa viongozi waliovishwa vyeo kubeba matumaini mapya katika utekelezaji wa majukumu ya uhifadhi, utalii na maendeleo ya jamii.

Jenerali Mabeyo ampongeza Waziri wa Maliasili na Utalii, Serikali kwa ujumla na wadau wa utalii walioiunga mkono hifadhi ya Ngorongoro na hatimae kutangazwa kuwa Kivutio Bora cha Utalii Afrika kwa mwaka 2025.




Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi NCAA Jenerali Venance Mabeyo (Mstaafu) akimvalisha cheo Mariam Kobelo kuwa Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi





# KAMISHNA BADRU ALA KIAPO CHA MAADILI.



Kamishna wa Uhifadhi, Mamlaka ya Hifadhi ya eneo la Ngorongoro (NCAA), Bw. Abdul-Razaq Badru tarehe 28 Juni, 2025 ameungana na viongozi wengine walioteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungaano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kula Kiapo cha Maadili katika hafla iliyofanyia Ikulu Chamwino Dodoma.

Akitoa ujumbe wake mara baada ya kuwaapisha viongozi wateule, Rais, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amemtaka Kamishna Badru kusimamia kikamilifu shughuli za Uhifadhi, kulinda Ikolojia, Uwekezaji na Maendeleo ya Jamii.

Dkt Samia amesema Ngorongoro ni Urithi wa Dunia hivyo ni lazima ilindwe kuhakikisha kwamba ikolojia yake inaimarishwa na kulinda rasilimali zilizopo na kuhakikisha kuwa umaarufu wake haupotei na kuongeza kuwa ana matumaini makubwa na Kamishna Badru kutumia maarifa yake, ujuzi na uzoefu wake katika kuisimamia Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro. Rais Samia alimteua Bw. Abdul-Razaq Badru kuwa Kamishna wa Uhifadhi NCAA tarehe 26 Mei, 2025.




# MAONESHO YA UTALII NA UWEKEZAJI ZANZIBAR YAWA FURSA KWA WANANCHI KUJUA VIVUTIO VYA UTALII NGORONGORO.

Na **Mustapha Seifdine, Fumba Zanzibar.**

Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) imeshiriki kwa mafanikio katika Maonesho ya Pili ya Utalii na Uwekezaji Zanzibar 2025, yaliyofanyika katika viwanja vya Dimani, Fumba Zanzibar, na kufunguliwa rasmi na Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mhe. Mudrik Ramadhan Soraga.

Kupitia ushiriki wake, NCAA imeendelea kuimarisha uelewa wa umma kuhusu umuhimu wa uhifadhi, utalii na fursa za uwekezaji zinazopatikana Hifadhi ya Ngorongoro ambalo ni eneo la kipekee duniani linalotambuliwa na UNESCO kama Urithi wa Dunia.

Akizungumza katika banda la NCAA, Bi. Zuhura Khalifa, mkazi wa Mkwajuni, aliipongeza mamlaka hiyo kwa kutoa elimu ya uhifadhi na taarifa za vivutio vya utalii vya Ngorongoro na kuvinadi katika visiwa vya Zanzibar.

“Watu wengi wamekuwa wakisikia kuhusu Hifadhi ya Ngorongoro, lakini hawakuwa na taarifa sahihi kuhusu huduma zake. Ushiriki wa NCAA katika maonesho haya umetufungua macho na umetufundisha mengi,” alieleza kwa furaha.

Kwa upande wake, Afisa Uhusiano wa NCAA, Mustapha Seifdine, amewashukuru wananchi wote waliotembelea banda la Mamlaka hiyo, akisisitiza kuwa ushiriki wa NCAA katika maonesho hayo ni muendelezo wa kusambaza taarifa sahihi kuhusu vivutio vya utalii na juhudi za uhifadhi.

“Tumejipanga kwa mkakati wa muda mrefu, si tu kutangaza vivutio vya Ngorongoro, bali pia kutoa elimu ya uhifadhi kwa wanafunzi wa shule za sekondari na vyuo nchini kote. Lengo letu ni kuhakikisha kaulimbiu ya ‘Tumerithishwa, Tuwarithishe’ inakuwa ya vitendo na endelevu,” alieleza Mustapha.






# NCAA ILIVYONOGESHA HAMASA YA UTALII WIKI YA UTUMISHI WA UMMA, DODOMA.

Na **Philomena Mbirika, Dodoma.**

> "
>
> Nimejisikia fahari kujua Tanzania tumebeba Historia adhimu Duniani ya Chimbuko la Mwanadamu, huu ni urithi mkubwa sana, natamani mimi na familia yangu tufike Laitole nikajione masalia hayo ya nyayo.
>
> **Bi. Theresia Steven**
> Mkazi wa Dodoma

Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) imeendelea kutumia fursa ya maonesho mbalimbali ikiwepo maadhimisho ya wiki ya utumishi wa umma yaliyofanyika Jijini Dodoma hivi karibuni kuhamasisha utalii wa ndani kwa wananchi na wadau mbalimbali waliofika kwenye banda la NCAA lililokuwa kwneye Banda la Wizara ya Mali Asili na Utalii.

Wananchi wa Mkoa wa Dodoma na Mikoa mingine waliofika kwenye banda la NCAA wamepata elimu na ufahamu juu ya shughuli mbalimbali zinazofanywa na NCAA kwenye Utalii, Uhifadhi na Maendeleo ya jamii huku wengi wakionekana kuvutiwa zaidi na vivutio vya Utalii vinavyopatikana Hifadhi ya Ngorongoro kama Bonde la kreta ya Ngorongoro, nyayo za Laitole, bonde la Olduvai George, Kreta ya Empakai, Mchanga unaohama na vivutio vingine.

"Nimejisikia fahari kujua Tanzania tumebeba Historia adhimu Duniani ya Chimbuko la Mwanadamu, huu ni urithi mkubwa sana, natamani mimi na familia yangu tufike Laitole nikajione masalia hayo ya nyayo". Alisema Bi. Theresia Steven mmoja wa wakazi wa Dodoma aliyetembelea banda la NCAA.

Akizungumza katika maonesho hayo, Afisa Utalii kutoka idara ya Huduma za Utalii na Masoko NCAA, Joseph Mzaga alieleza kuwa maadhimisho hayo ya wiki ya utumishi wa umma

yamewakutanisha na wadau mbalimbali na imekuwa fursa kwao kutangaza vivutio vya utalii ambako wananchi wameonekana kuwa na shauku ya kutembelea hifadhini hapo.

“Tumepokea wageni mbalimbali walioweza kufika kwenye banda letu ambao wengi wao walitamani kufahamu zaidi kuhusiana vivutio vya utalii, namna ya kufika hifadhini, viingilio na taarifa zingine Muhimu za kuwasaidia kwa ajili ya maandalizi ya safari zao” Alisema Mzaga.

Kwa upande wake, Bi. Agatha Antony ambaye ni mkazi wa Mkoa wa Dodoma aliyetembelea banda la NCAA alieleza kuwa maonesho hayo yamekuwa msaada mkubwa kwake na wenzake wanaopanga kutembelea Ngorongoro, kwa kuwa wamepata taarifa muhimu kuhusu gharama za kuingia hifadhini, njia za usafiri, na mambo ya kuzingatia kabla ya safari, jambo ambalo litawasaidia kujipanga vizuri na kuongeza hamasa kwao.

“Mimi pamoja na wafanyakazi wenzangu kutoka taasisi ya Pharma Afrika tunajiandaa na safari ya kutembelea hifadhi yaa Ngorongoro na leo nimefurahi zaidi kwani nimeweza kufika hapa na nimepata taarifa ambazo zitatusaidia kwenye maandalizi yetu mfano viingilio, usafiri na vivutio ambavyo tutaweza kuvitembelea.” Alisema Agatha.

Viongozi waliotembelea banda hilo ni pamoja na Naibu Waziri wa Maliasili na utalii Mhe. Dustan Kitandula (Mb) ambae alitoa wito kwa NCAA kuendelea kutoa Elimu kwa umma kuhusiana na jamii inayoishi ndani ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro kwa kulezea historia na asili halisi ya jamii hiyo. Aidha alisisitiza watanzania kuendelea kutembelea banda la Wizara ya Maliasili na Utalii katika maonesho mbalimbali ikiwemo sabasaba ili kupata elimu kuhusu shughuli za Uhifadhi, utalii na fursa za uwekezaji zinazopatikana katika sekta ya utalii.

Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yalifanyika tarehe 16 hadi 23 Juni 2025, ambapo mgeni rasmi alikuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb).






# MAPADRI KANISA KATOLIKI SINGIDA WAIASA JAMII KUTUNZA MAZINGIRA NA KUHAMASISHA UTALII WA NDANI.

Na **Walter Mairo, Dodoma.**

Mapadri 11 kutoka parokia mbalimbali za jimbo katoliki Singida mwezi Juni, 2025 wamefanya ziara ya kutembelea vivutio vya vya utalii katika hifadhi ya Ngorongoro na kusisitiza uhifadhi na utunzaji wa mazingira ili kuendelea kuvutia wageni wengi.

Kiongozi wa mapadri hao Padri John Makabe ameeleza kuwa, ziara yao imelenga kuona maajabu wa Mungu aliyoyaumba katika hifadhi ya Ngorongoro, vivutio vya utalii kama wanyamapori, malikale na mandhari mbalimbali zilizopo ili kwa nafasi zao wahamasishe jamii umuhimu wa uhifadhi na kutunza mazingira kwa manufaa ya wanadamu wote.

“Tumekuja kuona mazingira na kuhimiza utunzaji wake, neno la Mungu katika kitabu cha mwanzo tumeambiwa Mungu aliumba vitu vyote na kuwakabidhi binadamu ili wavitunze na kuvilinda, sisi watumishi wa mungu ni sehemu ya utume wetu kuelezea habari ya umuhimu wa kutunza mazingira, ziara yetu hapa Ngorongoro imetusaidia kuona ukweli wa maajabu ya Mungu kupitia hifadhi hii, tutaendelea kuhamasisha watu kutambua umuhimu wa mazingira kama zawadi tuliyopewa na mungu ili tuyatunze na yenyewe yatutunze kwa vizazi na vizazi” amesema Padri Makabe.

Akipokea ujumbe wa mapadri hao, Kamishna Msaidizi mwandamizi anayesimamia huduma za Utalii na Masoko Mariam Kobelo ameeleza kuwa hifadhi ya Ngorongoro imeendelea kupokea wageni wengi wa ndani na nje ya nchi na kubainisha kuwa jitihada za Serikali na wadau wa sekta binafsi kutangaza vivutio vya utalii nchini zimeendelea kuzaa matunda ambapo uongozi wa NCAA unahakikisha kuwa wageni wote wanapata huduma bora na kufurahia shughuli za utalii wanapokuwa ndani ya hifadhi.

# WAONGOZA UTALII WATOA KONGOLE KWA NCAA MABORESHO YA BARABARA KUELEKEA MSIMU WA UTALII.

Na **Philomena Mbirika, NCAA.**

Waongoza utalii kutoka kampuni mbalimbali zinazojihusisha na shughuli za utalii nchini wameipongeza uongozi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) kwa juhudi wanazofanya kuboresha miundombinu ya barabara katika Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro.

Wadau hao wameelezea hatua hiyo kuwa ni suluhisho la muda mrefu kwa changamoto zilizokuwa zikiwakabili, hasa wakati wa msimu wa kilele cha utalii (high season)

Wakizungumza kwa nyakati tofauti katika geti la kuingia hifadhi ya Ngorongoro, baadhi waongoza utalii hao wameeleza kuwa maboresho hayo yameleta mabadiliko makubwa katika usafiri, kupunguza muda wa safari, kuongeza usalama wa wageni, na kuboresha hali ya utalii katika hifadhi hiyo maarufu duniani.

"Tunatoa pongezi kwa NCAA kwa kazi kubwa waliyoifanya kuboresha barabara, kwa sasa imekuwa rahisi zaidi kuwafikisha wageni kwa haraka na salama kwenye maeneo ya vivutio vya utalii vilivyopo Ngorongoro
" alisema Mohammed Tenga kutoka kumpuni ya Zara Tours.

Kwa upande wake Walter Temba kutoka kampuni ya utalii ya Serengeti Smiles alieleza kuwa maboresho ya miundombinu ya barabara yanayoendelea yamekuja kwa wakati muafaka, ikizingatiwa kuwa sekta ya utalii nchini inaendelea kukua kwa kasi huku idadi ya wageni kutoka ndani na nje ya nchi ikiendelea kuongezeka kila mwaka.

"Kwa muda mrefu tumekuwa tukikumbana na changamoto kubwa hasa wakati wa mvua magari yanakwama na wageni kuharibika hata kabla ya kufika kwenye vivutio. Lakini sasa hali ni tofauti kabisa, barabara zimekarabatiwa kwa kiwango kizuri na zinaweza kupitika hata kipindi cha mvua ombi letu ni kuwa jitihada hizi ziwe endelevu," alisema Temba.

Kwa Mujibu wa NCAA, maboresho ya barabara ni sehemu ya maandalizi ya taasisi hiyo kukabiliana na ongezeko kubwa la watalii ambalo limeanza mwezi juni ambalo linatarajiwa kuongezeka hadi mwezi Oktoba kila mwaka.

Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro hupokea maelfu ya wageni kutoka mataifa mbalimbali duniani wanaokuja kutembelea vivutio vya utalii ambapo takwimu zinaonesha kuwa kati ya Mwezi Julai 2024 hadi Juni, 2025 jumla ya watalii 1,061,620 ikijumlisha watalii wa ndani 419,166 na watalii wa nje 642,454 wametembelea hifadhi kwa shughuli za utalii.





# NIDHAMU NA UADILIFU NI NYENZO MUHIMU KATIKA UTENDAJI KAZI KIJESHI; CP WAKULYAMBA.

Na **Kassim Nyaki, Karatu - Arusha.**

> "
> Natumia fursa hii kuwapongeza wahitimu wote 25 kwa kuhitimu mafunzo haya muhimu ya mabadiliko ya utendaji, hakikisheni mnazingatia, maadili, uadilifu, ujasiri, uzalendo, nidhamu, uadilifu kuzingatia amri na nidhamu za kijeshi na kuongeza ubunifu katika usimamizi wa rasilimali za misitu na wanyamapori na kuhakikisha kuwa mnaendelea kupata mafunzo ya mara kwa mara na kutumika ipasavyo katika maeneo yenu
>
> **CP. Benedict Wakulyamba**
> NKM, Wizara ya Maliasili na Utalii anayesimamia Maliasili

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii anayesimamia Maliasili CP. Benedict Wakulyamba amefunga mafunzo ya Afisa na Askari wa Jeshi la Uhifadhi NCAA yaliyofanyika katika kituo cha Mafunzo ya jeshi la Uhifadhi Mbulumbulu Wilaya ya Karatu Mkoani Arusha na kuhimiza nidhamu na uadilifu katika utendaji kazi kwa wahitimu hao.

Akifunga mafunzo hayo yenye wahitimu 25 wanaojumuisha Naibu Kamishna mmoja (01), Makamishna Wasaidizi waandamizi wanne (04), Maafisa Uhifadhi wakuu kumi (10), Afisa Uhifadhi waandamizi watano (05), afisa uhifadhi daraja kwanza wawili (02), askari uhifadhi mkuu 01 na askari uhifadhi daraja la pili (02) CP. Kamishna Wakulyamba amewasisitiza wahitimu hao kuzingatia uwajibikaji katika Utumishi kwa kufuata taratibu, nidhamu ya kijeshi na uzalendo katika kuitumikia nchi huku akisisituza watumishi hao kutumia vyeo walivyonavyo kama nyenzo ya utawala katika mfumo wa Kijeshi.

"Natumia fursa hii kuwapongeza wahitimu wote 25 kwa kuhitimu mafunzo haya muhimu ya mabadiliko ya utendaji, hakikisheni mnazingatia, maadili, uadilifu, ujasiri, uzalendo, nidhamu, uadilifu kuzingatia amri na nidhamu za kijeshi na kuongeza ubunifu katika usimamizi wa rasilimali za misitu na wanyamapori na kuhakikisha kuwa mnaendelea kupata

mafunzo ya mara kwa mara na kutumika ipasavyo katika maeneo yenu" alisisitiza Wakulyamba.

Akitoa taarifa kuhusu mafunzo hayo Mkuu wa Mafunzo hayo Kanali Fikiri Machibya amebainisha kuwa mafunzo kwa maafisa na askari waliohitimu yalijikita katika Uongozi wa kijeshi, Kwata, matumizi ya Silaha ndogo (SMG & PistoL, Itifaki na maadili, Ulinzi wa viongozi, General order (GO) na ulengaji shabaha.

Akizungumza kwa niaba ya Kamishna wa Uhifadhi Naibu kamishna wa Uhifadhi NCAA, Joas Makwati ameeleza kuwa mafunzo yaliyotolewa kwa watumishi hao ni fursa kujifunza kwa nadharia na vitendo juu ya mabadiliko ya mfumo wa kiraia kwenda katika mfumo wa kijeshi.

Makwati ameongeza kuwa mafunzo hayo yamewabadilisha viongozi, maafisa na maaskari wa uhifadhi katika kuwajibikaji kwenye majukumu ya kila siku kwa kuzingatia misingi ya kijeshi, nidhamu na utiifu na kubainisha kuwa uongozi wa NCAA utaendelea kuendesha mafunzo ya mara kwa mara kwa maafisa na askari wa jeshi la uhifadhi.

Mratibu wa Jeshi la Uhifadhi kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii Kamishna Msaidizi Mwandamizi Fidelis Kapalata ameeleza kuwa Wizara hiyo inaendelea kuhakikisha kuwa watumishi wote wa taasisi za Uhifadhi zilizoko chini ya Wizara hiyo zinaendelea kupata mafunzo ya mara kwa mara ili kujiimarisha katika udhibiti wa vitendo vya ujangili na kuwa imara mda wote katika kuzilinda rasilimali za wanyamapori na misitu.










# DKT. KIJAJI AZINDUA CHANJO YA MIFUGO NGORONGORO.

Na **Kassim Nyaki, NCAA.**

Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb) amezindua zoezi la Chanjo ya Mifugo katika Kijiji cha Mokilal Tarafa ya Ngorongoro Mkoani Arusha ikiwa ni utekelezaji wa mpango wa kitaifa wa miaka mitano wa kuchanja mifugo.

Dkt. Kijaji ameeleza kuwa katika utekelezaji wa zoezi hilo ambalo ni mpango wa kitaifa wa Miaka mitano kuanzia 2025-2030 ulizinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan tarehe 16 Juni, 2025 Bariadi Mkoani Simiyu na tayari kiasi cha shilingi bilioni 216 zimetengwa kufanya kazi hiyo na mwaka huu zaidi ya Bilioni 62 imeshatolewa.

Amesema kuwa Serikali imetoa punguzo la bei na kila Ng'ombe mfugaji atachangia shilingi 500 badala ya shilingi 1000 na Mbuzi na Kondoo wafugaji watachangia shilingi 300 pekee badala ya shilingi 500 ambapo mpango huu unalenga kuwasaidia wafugaji.

Mkurugenzi wa huduma za Mifugo kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi Benezeth Lutege ametaja Sababu za kuchanja mifugo hiyo kuwa ni Kuongeza thamani mifugo kwenye masoko ya nje, kujua idadi ya mifugo na wamiliki wake ili kurahisisha upangaji wa maeneo ya malisho na sababu nyingine kuwasaidia amana katika vyombo vya kifedha kupata mikopo kwa kuwa taarifa za mifugo yao itakuwa inatambulika mifumo ya kielektroniki (barcode) kupitia alama ya hereni za utambuzi kwa kila mmiliki wa mifugo.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Arusha Mhe. Kenan Kihongosi ameeleza kuwa Wananchi wa Ngorongoro na Mkoa wa Arusha kwa ujumla wamekuwa na muitikio mkubwa katika zoezi hilo na wataendelea kuhamasisha wafugaji wote kuchanja mifugo yao ili kutimiza azma ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuboresha maisha ya Wananchi

Mbunge wa Ngorongoro Mhe. Emmanuel Shangai ameishukuru Serikali kwa kuwasikiliza Wafugaji na kuwapatia chanjo ya mifugo yao na kuwaomba Wananchi wote kujitokeza kuchanja mifugo hiyo ili kuondokana na maradhi mbalimbali, kuboresha afya na thamani ya mifugo yao.

# HABARI PICHA

Baadhi ya Picha za Wakurugenzi wa Bodi ya NCAA wakiwa na Tuzo ya WTA iliyotunukiwa kwa Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro (NCA) baada ya kuibuka na ushindi wa kuwa Kivutio bora cha Utalii Afrika kwa mwaka 2025.



























Picha za matukio mbalimbali katika maonyesho ya Sabasaba yanayofanyika jijini Dar es Salaam

















# TAARIFA KWA UMMA

Dar es Salaam, Tanzania                                                    Tarehe: 28 Juni, 2025

## ENEO LA HIFADHI YA NGORONGORO LASHINDA TUZO YA KIVUTIO BORA BARANI AFRIKA 2025

**Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro (NCA)** limeshinda tuzo ya **Kivutio bora cha utalii Afrika kwa mwaka 2025** (Africa's Leading Tourist Attraction 2025) inayotolewa na mtandao wa **World Travel Awards (WTA)**.

"Tumepokea kwa furaha na hamasa kubwa tuzo hii, kwetu Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro imetuongezea ari ya kufanya kazi kwa juhudi na maarifa ili kulinda hadhi tuliyoipata na **tunawashukuru wale wote waliotupigia kura kwani imedhihirisha upekee wa eneo letu na bila kura zao tusingeweza kushinda**", **Abdul-razaq Badru, Kamishna wa Uhifadhi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.**

"Ngorongoro ni kivutio pekee duniani ambacho kina **hadhi tatu za Kimataifa** zinazotambuliwa na **UNESCO**, tunao Wanyama wakubwa maarufu watano "The Big Five' ambao ni faru, simba, tembo, nyati na chui sambamba na wanyama wengine wengi ambao unaweza kuwaona kwa pamoja na kwa utulivu ndani ya muda mfupi,tuna makumbusho ya kihistoria katika **Bonde la Olduvai** lilipogunduliwa Fuvu la

1/2

Binadamu wa kwanza 'Zinjanthropus', vivutio vingine ni pamoja na **nyayo za binadamu wa kale** aliyeishi zaidi ya miaka milioni 3.7 iliyopita, **mlima Lolmalasin** ambao ni wa tatu kwa urefu Tanzania, **mchanga unaohama**, **tambarare za Ndutu** ambazo ni mazalia ya nyumbu wanaohama, **maporomoko ya maji ya Endoro**, **mapango ya tembo** na mengine mengi", **msitu wa nyanda za juu kaskazini** ambao ni makazi ya Wanyama wengi na **chanzo cha maji wilaya za karatu, Monduli na Ngorongoro" Mariam Kobelo, Kamishna Mwandamizi Msaidizi anayeshughulikia Huduma za Utalii na Masoko.**

Mafanikio hayo yametokana na juhudi kubwa zinazofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan** kutokana na **hamasa kubwa aliyonayo katika sekta ya Uhifadhi na Utalii** hasa kupitia filamu ya *Tanzania: The Royal Tour na Amazing Tanzania.*

"Tuzo hii na nyingine tulizozipata ni mahsusi kwa Rais wetu mpendwa **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan** ambaye yeye ndiye **kinara wetu katika kusimamia uhifadhi, utalii na maendeleo ya watanzania, tutaendelea kulinda mafanikio haya kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho**", **Mhe. Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana, Waziri wa Maliasili na Utalii.**

Hii ni mara ya pili kwa eneo la Hifadhi ya Ngorongoro kushinda tuzo ya kuwa kivutio bora barani Afrika ambapo mara ya kwanza ilishinda tuzo hii mwaka 2023.

Imetolewa na;
**Abdul-razaq Badru**
**Kamishna wa Uhifadhi**
**Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA)**

Tripadvisor Travelers' Choice Awards Best of the Best 2024

Visit **NGORONGORO**
**for Unforgettable Experiences**

2/2


Visit NGORONGORO
for Unforgettable Experiences!
www.ncaa.go.tz
@visitngorongoro
TANZANIA
Unforgettable!